

# MILAMBO CO - OPERATIVE UNION LIMITED

MILAMBO CU(2018) LTD - REG. NO. AFF-TBR-URA-DC-2023-57

Telegraph: 'MILAMBO'

Tel:

Mob: 0765567584

Fax:

E-Mail: [milambocultd@gmail.com](mailto:milambocultd@gmail.com)



Bomani Road,  
P.O. Box 186,

**URAMBO.**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. AB.194/306/02/224

28 Februari, 2024

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Milambo CU Ltd,  
S.L.P 186,  
**URAMBO.**

**YAH: KUSOGEZWA MBELE KWA MKUTANO MKUU WA SITA (6) WA MILAMBO  
UNION AMBAO ULIKUWA UFANYIKE TAREHE 14-15 MACHI, 2024 NA  
SASA UTAFANYIKA TAREHE 15 – 16 MACHI, 2024 KATIKA UKUMBI WA  
ROMANI KATOLIKI – WILAYANI URAMBO.**

Tafadhali Rejeeni somo tajwa hapo juu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Milambo ameniagiza kuwatangazia kuwa Mkutano Mkuu wa sita (6) wa Milambo CU Ltd wa Mwaka utafanyika tarehe tajwa hapo juu siku ya **Ijumaa na Jumamosi kuanzia saa 2:00 Asubuhi** katika Ukumbi wa **Romani Katoliki – WILAYANI URAMBO.**

**Ajenda za Mkutano Mkuu wa Mwaka ni:-**

1. Kufungua Mkutano
  - i. Kusoma Tangazo la Mkutano Mkuu
  - ii. Kusoma masharti yahusuyo Mkutano Mkuu na kuthibitisha Akidi
2. Kuchagua Mwenyekiti wa Mkutano
3. Kuthibitisha Ajenda za Mkutano Mkuu
4. Kupokea wanachama wapya na kutoa vyeti kwa wanachama waliokamilisha mafungu (Hisa).
5. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano Mkuu uliopita
6. Kuwasilisha yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita
7. Kusoma na kujadili taarifa ya mkaguzi wa nje (COASCO)

8. Taarifa ya maendeleo ya shughuli za chama.
9. Kusoma na kuitisha makisio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha wa 2024/2025.
10. Kuteuwa mkaguzi wa nje kwa mwaka wa fedha wa 2024/2025
11. Uchaguzi wa viongozi wa Bodi ya Chama
12. Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
13. Kufunga Mkutano.

Wajumbe watakaohudhuria Mkutano huo ni wawili (2) kutoka kila Chama Mwanachama na wawe waliochaguliwa kuwakilisha vyama vyao katika Mkutano Mkuu wa Union (Mwenyekiti wa Chama cha msingi na Mjumbe mwakilishi).

Makatibu Meneja wa kila Chama Mwanachama wanakaribishwa kushiriki Mkutano kama waalikwa.

- Zingatieni:**
- (i) *Kwa chama cha msingi ambacho tangu kipokelewe kuwa mwanachama wa Chama Kikuu cha Ushirika Milambo kimeshatimiza miaka miwili (2) na hakijamaliza kulipa hisa zote tano (5) – hakihusiki na tangazo/mualiko huu.*
  - (ii) *Kwa Mwanachama mwenye mengineyo; ayawasilishe kwa barua ofisi ya Meneja Mkuu siku 14 kabla ya tarehe ya Mkutano Mkuu kufanyika.*

**“Pamoja na Salamu za Ushirika”**

Innocent J Tibesigwa  
**KAIMU MENEJA MKUU.**



#### **NAKALA KWA:-**

1. Mrasis na Mtendaji Mkuu,  
Tume ya Maendeleo ya Ushirika,  
S.L.P.201,  
**DODOMA.** – Unaombwa kuhudhuria
2. Mrasis Msaidizi (M),  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P.25,  
**TABORA.** – Unaombwa kuhudhuria
3. Afisa Ushirika (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Urambo  
S.L.P 170,  
**URAMBO.** – Unaombwa Kuhudhuria
4. Afisa Ushirika (w),  
Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua  
S.L.P 83  
**KALIUA.** – Unaombwa kuhudhuria